THE BRENTHURST FOUNDATION

*Strengthening Africa's Economic Performance*

# MJADALA WA BRENTHURST 2/2009

# Muafaka Wa Ziwa Kivu

## AJENDA KUHUSU AFRIKA KAKAMAVU


### MHUTASARI

### MIKAKATI KUMI YA KUBORESHA UKAKAMAVU WA AFRIKA

Muafaka wa Ziwa Kirvu ni matokeo ya majadiliano ya mikutano miwili iliyofanyika Italy na Rwanda mwaka wa 2008 ambapo ukakamavu ulitambuliwa kuwa wenye umuhimu sana katika mkakati wa Afrika kuongeza nafasi za ajira na ufanisi. Kuzorota kwa uchumi wa ulimwengu na kima cha uzazi Afrika chafanya jukumu hili lenye umuhimu mkuu kushughulikiwa kwa haraka.

Fasili ya ukakamavu katika stakabadhi hii ni hali ya kuwa na uwezo wa kuendeleza na kustawisha mazingira ambayo kampuni zaweza kuzalisha bidhaa na huduma ziwezazo kununuliwa katika soko huru.

Stakabadhi hii ya pendekeza hatua ambazo serikali za Afrika zafaa kuchukua zikishirikiana na sekta ya umma, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) na wafadhili (Donors) ili kuboresha ukakamvu wa uchumi wa bara hili:

1) **Sawazisha Marekebisho:** Zingatio lisiwe tu kwenye uchumi katika ukubwa wake (kama vile uadilifu katika hazina ya serikali, sera zinazohusu fedha na biashara) lakini marekebisho yawapo katika udogo wake, hasa katika sera zihusuzo ushuru wa serikali na matumizi, urahisishaji wa kuingiza au kufunga biashara pamoja na taratibu nyinginezo za kiserikali.
2) **Kupunguzwa Kwa Gharama, Vikwazo Na Mashaka: K**uondolewa kwa vikwazo vya kirasimu, kuekeza katika muundo msingi na ujuzi, na uhakika wa sheria na utangamano ni majukumu ya serikali. Nchi zisozoweza kuekeza katika afya, elimu au kulinda mazingira hawatakuwa na ukakamvu kwa muda mrefu.
3) **Alama Teule**: Ni lazima alama teule za ukakamavu zibuniwe kama njia mojawapo ya kulinganisha na kupunguza gharama ya kufanya biashara.
4) **Pambanua**: Huku changamoto za Afrika zikiwepo kote katika bara - nayo hali ya kukua ikiunganishwa na mali ghafi, gharama ya matumizi ikiwa ghali, kutokuwepo na miundo msingi bora, upungufu wa wenye ujuzi wa kazi, na nyongeza ya watu – kuwepo na serikali tofauti – zenye kuleta mabadiliko na zilizoanguka, wenye utajiri wa mafuta na maskini wa rasil mali, yalazimu mikakati ya ukakamavu kubuniwa kulingana na mahitaji ya nchi binafsi.
5) **Shindania Uekezaji, Sio Misaada**: Muda utolewe zaidi kwa serikali kushindania uekezaji, si kujadiliana kuhusu misaada watakayopokea. Jenga sehemu moja itakayoshughulikia yote yanayohitajika na kurahisisha taratibu kwa ajili ya waekezaji na sio wafadhili.
6) **Buni Kanuni Za Maadili Mema**: Kubali maadili mema ya biashara na mashirika yasiyo ya kiserikali. Katika hili, lenga kupunguza biashara zihitajizo jitihada nyingi na hakiki ubashiri wa mabadiliko simamizi na sera za ushuru.
7) **Ondoa uhusiano wa mabadiliko ya kinyumbani na msaada:** Serikali za Afrika sharti kufanya mabiliko yao binafsi ya kiuchumi bila ya kutegemea kuwepo kwa msaada. Kwa mfano, katika kuwepo kwa uwezekano wa kufanya biashara na mabadiliko ambatani, nchi zaweza kujimudu na kujifanikisha sana kwa msingi huu, kwamba wana viambato muhimu ambazo ni uongozi na usimamizi bora wa miradi na sio fedha.
8) **Dumisha Matumizi Muhimu**: Fanya kazi na taasisi za usimamizi wa fedha za kimataifa ili kuhakikisha kwamba matumizi ya serikali za kimsingi na muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi hazuiliwi.
9) **Hakikisha ukakamavu wa Fedha**: Ni lazima kujilinda dhidi ya "*Ugonjwa wa Kidachi"*(Dutch disease), na kuhakikisha ukakamavu katika ubadilishaniaji wa fedha
10) **Unda Muungano Wa Kukua Pamoja**: Fanya makubaliano kuhusu hitaji la mabadiliko ya kiuchumi, umuhimu wa uzalishaji zaidi ili kupunguza umaskini, na kuiunganisha nchi na uchumi wa ulimwengu.

Nchi za Afrika zitakazo kubalia na kutekeleza haya hazitakuwa tu na ukakamavu bali zitapunguza umaskini kwa kiwango kikubwa sana.

## UTANGULIZI: CHANGAMOTO YA KUENDELEA

Njia ya pekee ambayo nchi yo yote leo hii yaweza kuteseka mno, ni udhalimu wa kutengwa hasa kutoka kwa mikono ya uchumi wa ulimwengu. Kwa hivyo, marekebisho kwa lengo la kuwa wakakamavu ndio kipaumbele katika Afrika. Ila, ni lazima ieleweke kwamba hamna njia moja ya kuwa na ukakamavu wa kiuchumi. Basi, nchi zote zenye matamanio ya usoni ya kutotegemea misaada ni lazima kubaini shida zilizoko na kubuni suluhu dhidi ya yanayowazuia kutoshiriki katika biashara ya ulimwengu.

Jukumu la kufanya uchumi wa Afrika kuwa kakamvu ni hitaji lisiloweza kusubiri.Bidhaa zenye mauzo ya juu zilizo himili kukuwa kwa kiasi cha asili mia tano kwa mwaka katika miaka iliyopita, sasa imepungua sana. Kadri ya mapato ya serikali za nchi zilizoendelea zinavyopungua, ndivyo msaada kwa serikali za Afrika utaendelea kupungua. Pia, kutakuwepo na upungufu wa Waafrika walioko ng'ambo kutuma fedha, ambayo ni mojawapo ya chanzo kikuu katika uekezaji na ustawi wa jamii.

Uhalisi wa mambo ukiwa jinsi hii, yaonyesha umuhimu wa kuongeza thamani zaidi kwa mauzo nje ya Afrika, kuezeka katika umma hasa katika ujuzi, na katika taasisi mbali mbali, na pia kubadili mawazo ili kuwezesha Afrika ishiriki katika uchumi wa ulimwengu. Hitaji lililopo ni kuunda muungano wa kukuza uchumi katika bara la Afrika, ili uwezo wa sekta ya kibinafsi, iliyo na uwezo wa kutenda mema katika jamii, ipate kueleweka vyema na Waafrika wanaofanya maamuzi ya kutunga sera, wenye maoni yenye ushawishi, na makundi ya umma miongoni mwa wengine.

Shinikizo la ndani kwa ndani laendelea kuleta msukumo wa utekelezaji na mabadiliko. Ifikiapo mwaka wa 2025, kati ya vijana wanne ulimwenguni, mmoja atakuwa yuatoka kusini mwa Sahara, hivyo kufanya asili mia 40 ya wenye uwezo wa kufanya kazi, huku asili mia 60 wakiwa bila ajira. Umaskini na hali duni ya maisha, na ukosefu wa huduma za kimsingi pamoja na pengo kubwa kati ya walio matajiri na masikini ni msingi wa vurugu na ghasia katika umma. Kutengwa kwa wanawake wa Afrika katika juhudi za kiuchumi huzuia maendeleo zaidi. Ikiwa talanta zao zitafunguliwa, wanawake wa Afrika na vijana watachochea mabadiliko mazuri katika bara hili; wakipuuziliwa basi shida zao zitakuwa chanzo cha mizozo ya kijamii na kisiasa.

Miaka 25 iliyopita, ajenda ya marekebisho yametiliwa mkazo na kuendeshwa kulingana na matakwa ya wafadhili. Sera ziliundwa kulingana na lile liitwalo 'Muafaka wa Washington' (Washington Consensus), iliyosisitiza nidhamu upande wa ukubwa wa uchumi (jambo ambalo Afrika ilitunza), pamoja na kuwepo kwa soko huru (jambo lililokwepwa sana). Mjadala huo baadaye ulielekezwa kujadili kuhusu usimamizi na taasisi zikiwa upande mwingine ikiakilishwa na Ushirika mpya wa maendeleo ya Afrika (NEPAD), na kuekeza pakubwa katika 'mtaji wa kibinadamu' (human capital) kama ilivyopewa kipaumbele katika malengo ya milinia ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UN Millennium Development Goals). Hivi majuzi, Afrika imetizama uchumi wa Uchina jinsi umekuwa kwa haraka, na kujiuliza iwapo kumekuwapo "Muafaka wa Beijing' (Beijing Consensus), unaoweza kutumika kama chaguo jingine.

**MUAFAKA WA WASHINGTON**

John Williamson ndiye alibuni jina hili, 'Muafaka wa Washington'. Aliakilisha sehemu kumi za marekebisho ya kile ambacho wengi wa wahusika katika taasisi ya kimataifa ya usimamizi wa fedha waliamini kwamba Marekani ya Kusini (siyo nchi zote) walifaa kutekeleza kufikia 1989 (ila si kila wakati). Wazo hili lilijumuisha nidhamu katika usimamizi wa hazina ya serikali, kuwa na ukakamavu katika ubadhilishaji wa fedha za kigeni, kuidhinisha soko huru na ubinafsishaji wa mashirika.

Williamson alikuwa na 'mambo matatu makuu' aliyoona kuwa ni msingi wa muafaka huo. Mambo hayo ni kama ifuatavyo: nidhamu katika ukubwa wa uchumi; uchumi unaotegemea soko huru na uwazi kwa ulimwengu kwa habari ya biashara na uekezaji.

Licha ya kelele zilizopo, Afrika imejisatiti kueleza kwa ufasaha ajenda yake. Hali iliyopo wasiwazi kuhusu uchumi na usalama imeongezea katika udhaifu wa serikali za kiafrika na kufanya pawepo na ugumu mkubwa wa kubuni na kutekeleza marekebisho. Mbali na wachache, sehemu zenye kupendelea marekebisho bado hazijaebuka po pote katika bara la Afrika,

Muafaka huu ulitokana na msingi kwamba, uboreshaji wa ukakamavu wa kiafrika ni muhimu kwa maendeleo. Changamoto haikuwa kubisha kuhusu umuhimu wa mjadala, bali ni kuelezea kinachohitajika na jinsi ya kukifikia.

Muafaka huu ni matokeo ya ushirikiano kati ya Taasisi ya Brenthurst, Ubia ya taasisi ya uchunguzi wa kiuchumi Afrika, Uongozi wa Wanabiashara Afrika Kusini, na shirika la Konrad-Adenauer-Stiftung. Shughuli

hii iliwakutanisha wafanya biashara, waundaji sera, waandishi wa habari, wasomi, na viongozi katika dhana kwenye mkutano uliokuwepo Villa La Collina, Cadenabbia, Italia tarehe 26 – 28 Mei, 2008., na baadaye kwenye fuo za Ziwa Kivu, Gisenyi, Rwanda. tarehe 14-15 Desemba, 2008. Majina ya walioshiriki utayapata katika kiambatisho.

## CHANGAMOTO KUHUSU UKAKAMAVU WA AFRIKA

Shida kuu inayoadhiri maendeleo ya Afrika ni ugumu wa kufanya biashara huko. Kulingana na toleo la Benki ya Dunia ya mwaka, '*Uchunguzi wa Kufanya Biashara'* Afrika yahesabiwa kuwa bara lenye ugumu na vikwazo kwa wafanya biashara. Nchi za Afrika yaorodheshwa kuwa ya nambari 138 wastani, ikilinganishwa na nambari 87 ya nchi za Amerika Kusini (Kilatini) na za Caribbean. Kwa Afrika kusitirika siku za usoni, na kuimarishwa, tegemeo ni kuondoa vikwazo vinavyopunguza au kuzuia ukakamavu katika sekta ya kibinafsi – hasa vikwazo vinavyotokana na bunifu usio na busara wa serikali.

Ukakamavu wa nchi ni ule uwezo wa nchi kuendeleza mazingira yatakayowezesha viwanda kutengeza bidhaa kwa faida na kutoa huduma ziwezazo kununuliwa katika soko. Kuondolewa kwa vikwazo vy kirasimu, kuekeza katika muundo msingi na ujuzi, na kuhakikisha kwamba kuna utawala wa sheria ni majukumu muhimu ya serikali yo yote ile. Bila shaka, nchi zisizoekeza katika kulinda mazingira, afya, na elimu hazitaendelea kuwa kakamavu kwa muda mrefu.

Mabadiliko mawili yamekuwepo katika Afrika ambayo yaturuhusu tuzingatie ukakamavu. Kwanza, demokrasia imesambaa sana wakati huu tangu nchi nyingi zijipatie uhuru. Jambo la pili ni kwamba Afrika imefurahia maendeleo ya kiuchumi, ambayo imepunguza pingamizi dhidi ya marekebisho katika soko huru.

**HISTORIA YA UCHUMI WA AFRIKA**

Ingawaje ni vigumu kujumulisha nchi arobaini na nane, ila Afrika iliyoko kusini mwa Sahara historia ya uchumi baada ya ukoloni waweza kugawanywa mara tatu. Katika miaka ya 1960s, uchumi ya nchi za Afrika zilikua kwa msingi wa bei ya juu kutokana na rasil mali za kila nchi Mapato kwa kila mtu iliongezeka katikati ya miaka ya 1970s.




Baadaye muda wa mapato kuteremka chiini ilifuatia hadi katikati mwa miaka ya 1990s, kwa sababu ya bei ya mafuta, bei ya chini ya mali ghafi na uharibifu wa uchumi kutokana sera mbaya kutoka kwa serikali. Kwa miaka kumi na mitano sasa, kiwango cha uchumi kimeinuka kutokana na marekebisho ya kiuchumi na hitaji la mali ghafi ya bara hili. Hata hivyo mapato ya wastani kwa kila mtu i chini ya kiwango kilichokuwepo katikati mwa miaka ya 1970.

Demokrasia katika hali yake ni muhimu kwani huendeleza kukua kwa uchumi na hali ya jamii. Utafiti wa hivi karibuni waonyesha kwamba zaidi ya miongo miwili iliyopita, asili mia 65 ya nchi zilizotawaliwa na madikteta zilikuza uchumi wake, huku theluthi moja ya jumla ya hesabu hii walirekodi mwaka mmoja wa kuzorota kwa uchumi. Kati ya nchi zinazoendelea nje ya Asia Mashariki, kati ya mwaka wa 1960 – 2003, nchi zenye mwongozo wa kidemokrasia zilikuza uchumi wao kwa asili mia 50 kasi kuliko zilizoongozwa kwa kiimla au udikteta.

Nchi zenye muongozo wa kidemokrasia hupunguza gharama kwa kukwepa ghasia na mapigano, kuboresha hali ya umma kuangalia kwa umaakini matumizi ya serikali, na kufanya serikali kuwajibika sana. Nchi kama hizi hufanya vyema kwa kuunda 'Taasisi za uwajibikaji' zenye kutekeleza sheria, kuzuia utumizi mbaya wa mamlaka katika serikali, kuzuia ufisadi, na kutenganisha uaminifu wa kisiasa na utumishi kwa umma.

Muongozo wa kidemokrasia una uwezo wa kuendeleza makubaliano ya kisiasa kuhusu marekebisho yanayobainisha kati ya marekebisho yaliyofanikiwa na hayo yaliyoshindwa. Sababu ya Afrika kuwa maskini zaidi tangu uhuru si kwamba walipata ushauri mbaya, lakini ni kwa kuwa nchi chache walifanya makubaliano ya wao kwa wao, kuhusu marekebisho na kuikuza sekta ya kibinafsi. Marekebisho muhimu huwa chungu kisiasa kwani hulazimu serikali kuvua mamlaka yake ili itwaliwe na soko na hao walioko kwenye sekta ya kibinafsi. Hii ni kwa kuwa wao huwapa changamoto mashirika yenye ukiritimba na yenye kulindwa kutokana na ushawishi wa kisiasa.

**MEXICO: MFUATANO WA MAREKEBISHO, KUKABILIANA NA ,KUKABILIANA NA MASLAHI**

Nchi ya Mexico imefanya mabadiliko makuu sana katika nusu karne iliyo pita. Kutoka kwenye nchi iliyokuwa na uchumi uliojitegemea na mfumo wa kisiasa usiokuwa wazi, na kufanyika kuwa nchi yenye maongozo ya kidemokrasia, yenye sarafu dhabiti, nchi hiyo imeorodheshwa kuwa ya kati ya kumi na tano ulimwenguni katika kuteneza mapato zaidi, na kukuza uchumi. Mwaka wa 1994, Mexico ilianza kuungana kiuchumi na Marekani na Canada, katika lililojulikana kama Biashara huru ya Amerika Kaskazini (NAFTA).

Kwenye mwaka wa 2000 Vincent Fox alichaguliwa kuwa rais, naye akakomesha ukiritimba katika sekta ya umeme iliyosimamiwa na Taasisi ya Chama Cha Mageuzi (PRI). Kwenye mwaka wa 2007, raia wa Mexico waliokuwa wakiishi ng'ambo, hasa Marekani na Canada, walituma nyumbani, nchi yao, kiasi cha kushangaza cha dola za kimarekani bilioni ishirini na nne (US$24b). Mapato hayo yalikuwa njia mojawapo kuu sana ya mapato ya fedha za kigeni, iliyoendesha biashara zaidi ya taifa hilo – kwa dola nyingi kuendelea kutumwa,

Katika hali ya kukubalia mabadiliko katika siasa, na muundo wa uchumi wa Mexico serikali nyingi katika miaka 20 iliyopita zimechagua kuchukua hatua mbili kwa kutekeleza malengo yao. Kwanza, ni uamuzi wa kuwepo kwa soko huru na kujiunga katika utaratibu wa kufanya biashara katika ulimwengu {GATT ambayo ilibadilishwa na kuitwa Shirika la Biashara Ulimwenguni (WTO)}, wakiafikiana na kukubaliana kuhusu soko huru na washirika wakuu katika biashara, na kujiunga na mashirika ya Ushirikiano wa kiuchumi na Maendeleo (OECD), jopo la Ushirikiano wa Kiuchumi wa Asia – Pacific (APEC) miongoni mwa shirika nyinginezo. Wakati huo huo, marekebisho yalifanyika ya kimsingi hadi kwa habari ya sheria ya umiliki wa akili mali, sheria, ukodeshaji wa nchi, sheria za uchaguzi, na marekebisho katika hazina ya serikali ikawa msingi wa kuifanya nchi hiyo kuwa na utayari wa uekezaji wa moja kwa moja kutoka kwenye nchi za kigeni na pia kuwa wazi kwa taratibu za biashara ulimwenguni. Hatua ya mwisho ilihusu sheria za kuhakikisha uwazi na usimamizi bora katika sekta ya umma na ile ya umma/binafsi katika ushirikiano wa kuezeka katika muundo msingi. Mabadiliko haya ya kimsingi katika uchumi wa Mexico na hali ya kisiasa iliwezesha nchi hii kuwa na vifaa vinavyohitajika vya kuwa wakakamavu, na si tu kati ya jirani zake, yaani Marekani ya Kaskazini na Marekani ya kusini tu, bali pia bara Ulaya na Hindi.

Kazi ya ndani kwa ndani ya kisiasa ni kitobu kinachoepukwa sana hasa kuhusu 'umiliki', nayo yajulikana kama '*Jambo la lazima*' (*sine qua non)* ili kuwepo na ufanisi na maendeleo ya kudumu. Wageni hawawezi kuiteneza, na hakuna nchi iwezayo kufanikiwa bila hiyo.

**EL SALVADOR: MAENDELEO KUTOKA KWA NCHI ISIYO NA SIASA IMARA**.

El Salvador yaonyesha jinsi yaliyopita si utangulizi. Yawezekana kukabili historia yenye udhalimu, siasa kingamizi, ugavi mbaya wa utajiri, uhalifu, kuharibiwa kwa misitu na tegemeo tu kwa ukulima. Pia yawezekana kubadili sehemu iwe yenye manufaa sana.

Watu yapata 75,000 walikufa katika vita vya wenyewe kwa wenyewe, na gharama ikifikia US$5 bilioni. Jumla ya Pato la taifa lilitelemka kwa kiwango cha asili mia 20. Hata hivyo, ilichangia pakubwa marekebisho katika nyanja ya siasa na uchumi baada ya mapatano ya amani kwenye mwaka wa 1992, huku demokrasia ikiwa msingi na mnara wa kujijenga upya. Tangu wakati huo, El Salvador imefuata kwa uadilifu marekebisho ya kiuchumi ikiwemo ubinafsishaji, marekebisho katika ushuru, na uhuru wa kutumia dola ya kimarekani kuidhinishwa kwenye mwaka wa 2001 ikifuatiwa na kuwepo kwa soko huru.

Mapatano ya uhuru wa biashara ya Amerika ya kati imeanza kuzalisha matokeo, kwa kuondoa kodi zote na vikwazo vya kuezeka dhidi ya Marekani na nchi nyingine tano za Marekani ya kati

Jumla ya Pato la taifa la mwaka la nchi ya El Salvador imekua hata kufikia asili mia tano baada ya kukwama kwenye asili mia moja nukta tano. Serikali imechukua usimamizi wa miradi maalum hivyo kuongezea kukua kwa uchumi. San Salvador, mji mkuu wa El Salvador umebadilika na kuwa wenye umuhimu sana katika eneo hilo. Safari za kuunganisha za ndege kutoka Marekani kusini hadi Marekani Kaskazini zafanyiwa hapa, Amerika ya kati imejumuishwa hapa. Uekezaji katika kuitangaza El Salvador imeiwezesha kuvutia wawekezaji wa viwanda vyenye teknolojia ya hali ya juu. Mfano ni kampuni ya kompyuta iitwayo Dell iliyojenga afisi za kutafsiri Kiingereza katika lugha ya kihispania, ili kutumika katika simu! Sekta ya fedha nayo iliuziwa benki za kimataifa, huku waekezaji wengi wakitoka Ulaya na Marekani, nao wamiliki kama vile viwanda vya kuunda mvinyo, saruji, usimamizi wa hazina ya uzeeni, kampuni za bima miongoni mwa nyingine zaidi. Takriban US$3 zimeezekwa katika nchi hiyo tangu mwaka wa 2005.

El – Salvador ilikuwa na nafasi kidogo tu ya kuteneza mipango yake ya usoni, ikionyesha kwamba, zaidi ya yote, wokovu ni lazima kutoka ndani. Hili ni himizo kwa serikali za kiafrika zinazoinuka kutoka kwenye miaka ya vita, zisizokuwa na mengi ya kuchagua ili kuiendeleza nchi, ila kuhitaji msaada zaidi. Iwapo El – Salvador ilikuwa imeharibiwa kwa ajili ya vita yaweza kujimudu, kwa nini isiwe nchi za kiafrika?

Kwa bahati nzuri kuna uwazi kwa habari ya marekebisho ya kiuchumi leo katika Afrika. Kati ya mijadala muhimu ni hitaji la kuwepo na ukakamavu katika ubadilishanaji wa fedha za kigeni, umuhimu wa sekta ya kibinafsi, na uhusiano kati ya serikali na Soko huru zaendelea kuondosha utata miongoni mwao japo suluhu kamili haipo.

Lakini, baada ya kufanya uamuzi mgumu, baadhi ya nchi katika Afrika sasa zafurahia faida kwa kuwepo na ongezeko la uekezaji wa kigeni na wa raia wake. Wengi barani wafanya bidii kuhakikisha kwamba wamefuata mifano hiyo, na kuweka matofali mahali panapohitajika.

**ZAMA YA GEORGIA**

Tangu Mageuzi ya Waridi (Rose Revolution) katika nchi ya Georgia kwenye mwaka wa 2003, Georgia imekuwa kielelezo cha marekebisho, ujenzi wake ukiwa katika nyongeza ya uhuru, na kuboresha ukakamavu, hii ikijumuisha ubinafsishaji wa maelfu ya viwanda vilivyo milikiwa na serikali, kubadili sheria ya ushuru kwa mashirika na kuifanya kuwa asili mia 15 (awali ilikuwa asili mia 47) kufutilia mbali ushuru utokanao na faida, riba, na magawio, jambo lililofanya mapato ya serikali kuongezeka. Kati ya soko zilizowazi, Georgia ni mojawapo (Kwa mfano, ushuru unaotozwa bidhaa za kuagiza kutoka nje ya nchi hiyo ni sawa sawa na ile ya Singapore na Hong Kong – nchi ambazo Georgia ili iga sheria zake ilipokuwa ikifanya marekebisho katika sheria).

Kwa kuondoa habari za usajili wa leseni, na stakabadhi nyinginezo zilizohitajika katika ujenzi na kufanya biashara, na kwa kuhitaji serikali ijibie swala lo lote kwa muda uliotengwa (Kawaida ni wiki mbili), Georgia ilivunja rekodi katika kupunguza ufisadi katika kila daraja.

Kusudi la serikali na lengo lake imekuwa kuhakikisha kwamba kuna mazingira ya kukuza na kuendeleza biashara wala siyo kupendelea sekta fulani kwa kuipigia debe. Uchumi hujakua tu katika huduma kama vile utalii, bali hata kutoka kwenye sehemu zisizotarajiwa kama vile upandikizi wa nywele yenye soko kule Korea Kusini.

Georgia ni kielelezo cha uhuru wa kiuchumi, hasa kwa kufanya marekebisho peke yao bila hofu ya matokeo yanayofanya nchi nyingi kuhofu kufanya hivyo. Nchi hii imeondoa masharti ya kibali cha usafiri kwa nchi karibia 50, yatambua na kuafikiana na taratibu za kiteknolojia na ukaguzi wa nchi zilizoko shiriki katika OECD na muungano wa nchi za Ulaya hivyo kuondosha hitaji la usajilishaji upya wa Georgia. Georgia hutumia taratibu hii kupata maelezo mafupi ya taratibu zihusuzo fedha.

Kwenye mwaka wa 2007 Georgia iliorodheshwa kuwa bora ulimwenguni kwa habari ya urahisi uliopo wa kufanya biashara katika nchi ile kulingana na takwimu za Benki ya Dunia. Ilipanda kutoka kwenye sehemu ya 112 hadi ya 37 katika muda wa mwaka mmoja, maendeleo makubwa sana. Tena kati ya mataifa 178, kufikia nambari 18, kwenye mwaka wa 2008. Idadi ya leseni zinazohitajika kufanya biashara zimepungua pakubwa kwa kiwango cha mara kumi. Kulingana na Benki ya Dunia, kati ya mwaka wa 2002–2005 ufisadi ulipunguka kwa kiwango kikubwa mno katika nchi ile. Matokeo yalikuwa hivi, uchumi uliongezeka kwa asili mia 10, na umasikini miongoni mwa watu milioni 4.5 wa nchi hiyo kupunguka kutoka kwenye asili mia 54 katika mwaka wa 2001 hadi asili mia 34 katika mwaka wa 2006. Ingawaje uchumi umeumizwa mara mbili kutokana na mshtuko wa vita vya Agosti 2008 na Urusi, na hali ambatani ya kuzorota kwa uchumi katika ulimwengu, misingi ya ufanisi wa muda mrefu haikutikiswa bado ipo.

Aliyekuwa Waziri Mkuu, Bwana Lado Gurgenidze, asema hivi, kwamba, ‘Somo lililopo kwa wengine ni rahisi, ushuru uwe sawa kote, pasiwepo na vikwazo dhidi ya fedha za kigeni au serikali kusimamia mapato, uhuru wa soko na utendaji kazi, ondoa urasimu, usivumilie ufisadi wa namna yo yote, na uhakikishe usalama wa waekezaji.’ Mikakati hii in dhima isiyo kubwa, kuliko kufanya nchi iwe na woga, bali kufaidi zaidi.

Nchi zinazoendelea, ikijumuisha nchi ambazo wakati moja zilikuwa zembe kama vile India na Mexico – sasa zaonyesha jinsi marekebisho yaongoza pawepo na kukua kwa uchumi na nafasi za ajira kwa maskini. Hii ni funzo na himizo kwa Afrika, ingawaje pia ni onyo kwa Afrika kwamba imebakia nyuma huku ulimwengu ukiendelea kujiendeleza. Mikakati inayobuniwa na nchi nyinginezo zinazoendelea hatimaye zitafungia njia ambazo Afrika ingelitumia kukua, ingawaje njia nyingine zaweza kufunguka baadaye.

**INDIA: KUEPUKA KUKUA ‘KIHINDI’**

Hadithi iliyopo kuhusu uchumi wa India ni kwamba uliharibiwa kutokana na hali ya kutobadilika kwa uchumi huo kwa muda mrefu ukiwa kwenye asili mia 3.5, hadi marekebisho ya kiuchumi yalipojiri kwenye mwaka wa 1991. Japo wazo la kukua kihindi lilikuwa likisambazwa katika mwaka wa 1980, India ilikuwa imeinua uchumi wake kufikia asili mia 5.5 katika jumla ya mapato ya kitaifa. Hili lilikuwa hivi kutokana na ongezeko la kujiwekea hazina katika uchumi na pia kuezeka humo hadi kufikia asili mia 25 (Kutoka asili mia 10 wakati wa kujinyakulia uhuru kutoka Uingereza mwa wa 1947). Licha ya marekebisho yaliyoanza mwaka wa 1991, India ilisalia chini ya asili mia 6 ya jumla ya mapato ya kitaifa hadi miaka tano iliyopita (2003 – 8), ambapo kiasi kinachohitajika kilizidi asilimia 8.8 na hivyo kuifanya kuwa kati ya uchumi zinazokuwa kwa kasi ulimwenguni baada ya Uchina – Kwa kuwepo na nyongeza katika kuweka hazina na uekezaji hadi kufikia kiwango cha asili mia 35 ya jumla ya mapato ya taifa.

Marekebisho hayakuanza katika mwaka wa 1991. Marekebisho yalianza muongo mmoja hapo urasimu wa serikali ulipoanza kulegeza kamba zake pole pole katika viwanda na biashara nyinginezo. Kwa hivyo misingi ya ufanisi iliwekwa yapata kwenye miaka ya 1960 kwa kuanzisha taasisi za elimu ya juu katika teknolojia na usimamizi, na kuanzishwa kwa ‘*Mapinduzi ya kijani kibichi*’ iliyoadhiri kilimo na hivyo kufanya kuwepo na upungufu wa chakula. Wala wahindi wa mapato ya kati hawakutokea kwa ghafla. kundi hili lilikuwa kwa utaratibu (Kulingana na mtazamo wa kiwango cha Soko) hadi kufikia kilele chake katikati ya miaka ya 1980.

Muungano wa biashara kati ya nchi hufaidi nchi kwa kuwepo na bidhaa au huduma zenye bei nafuu. Nchi zinazoendelea zinazojifungua kwa uchumi wa ulimwengu hukuwa kiuchumi haraka. Hii haina maana kwamba kuchanganywa kwa biashara italeta usawa mara moja; kweli ni kwamba pengo katika mapato huenda likawa kubwa zaidi. Lakini uchumi wa kiulimwengu hupendelea sekta ya kinyumbani kwa wingi – katika kazi, mali ghafi, nchi, au mtaji – nayo Afrika imetunikiwa za kwanza tatu. Haifaidi Afrika kuwa na sera za kujilinda, ila kuina njia za serikali kusaidia viwanda vinavyokuwa na kupunguza mapato yasiyolingana.

**VIETNAM: KUWEKA SAWA KANUNI ZA KIUCHUMI**

Baada ya vita vya 1975, uchumi wa Vietnam ulikuwa umezorota kabisa na nchi kujulikana kwa wakimbizi waliokimbilia nyingi nyingine kwa wingi. Serikali ilianzisha uvumbuzi kuanzia mwaka wa 1986, ikitupilia mbali sera ya ujamaa katika kilimo, na kukumbatia umiliki wa kibinafsi, mabadiliko yamekuwa makubwa. Mabadiliko haya yamewafanya wengi waliokuwa wakimbizi, na waliokuwa wakiishi katika mitumbwi kurudi nyumbani kwa sababu ya tumaini lililopo katika Vietnam.

Muungano wa Sovieti ulipokuwa ukianguka, ulisitisha msaada wake kwa Vietnam katikati ya miaka 1980. Vietnam iliyokuwa wakati mmoja ya kwanza katika uzalishaji wa mchele ulimwenguni, ilijipata ikiagiza mchele zaidi ya tani 1.5 ya mchele kila mwaka ili kuzuia janga la njaa. Hali hii ya wasiwasi iliwapa waliokuwa na dhana za marekebisho katika chama cha kikomunisti fursa ya kuungwa mkono kisiasa ili kuondoka katika sera ya kuamuru uchumi na kugeukia uchumi unaotokana na soko.

Sera za kutangulia ziliidhinisha ugatuzi wa usimamizi wa kiuchumi wa serikali, na kuruhusu viwanda kujisimamia; badala ya kuwepo na usimamizi wa kirasimu mahala pake palichukuliwa na mikakati ya kiuchumi, hii ilijumuisha soko lililoelekezwa na sera ya fedha ilivyo saidia kudhibiti kuzorota kwa uchumi; sera ya kutazama nje ya nchi zilibuniwa hasa katika uhusiano wa nje wa kiuchumi, hii ilijumuisha kuruhusiwa kwa fedha za kigeni na riba kujibia hali iliyoko katika soko; kuimarishwa kwa sera simamizi katika sekta ya ukulima iliyoruhusu haki ya utumizi wa nchi kwa muda mrefu, uekezaji ulihimizwa; sekta ya kibanfsi iliegemewa kama kitovu cha kuendesha uchumi; Viwanda vya kiserakali na kibinafsi ziliruhusiwa kushirikiana moja kwa moja na waekezaji wa kigeni, kwa ajili ya biashara nje na uagizaji wa bidhaa kutoka nje. Uvumbuzi zaidi ulijumuisha marekebisho katika sheria ya uekezaji wa kigeni, kuondolewa kabisa kwa ruzuku na usimamizi wa bei, kufunguliwa kwa sekta ya benki kwa ushirika wa kigeni; kuundwa kwa sehemu maalum ya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya biashara nje zilizomilikiwa asili mia mia kwa umiliki wa kigeni. Kuvunjilia mbali urasimu wa mipango, na kuwarudishia wamiliki wa zamani au warithi wao biashara zilizokuwa zimetwaliwa au kutaifishwa baada ya muungano kwenye mwaka wa 1975, kwenye sharti kuwa watekeza katika biashara hizo.

Kutokana na marekebisho haya, sasa Vietnam ni ya pili katika ukuzaji na uuzaji nje wa mchele katika ulimwengu, pia ni ya pili katika uzalishaji wa kahawa aina ya Robusta. Kwa muongo mmoja uliyopita, uchumi ulikuwa kwa wastani ya asili mia 7.5, ikichochewa na uzalishaji wa bidhaa katika viwango mbali mbali kama vile viwanda vidogo vyya kutengeneza nguo hata kufikia uekezeji wa aina yake kutoka kwa kampuni kuu ya kompyuta iitwayo *Intel* uliyotumia dola bilioni 1.3 za kimarekani. Zaidi, mbali na jirani zao 1.3 bilioni walio kaskazini mwa nchi yao katika Jamhuri ya Wat wa Uchina, watu wa Vietnam wapatao milioni 86 wamefanya juhudi ya kupunguza umaskini miongoni wao na kudumisha mshikamano wa jamii. Kwa mfano ‘*Vietnam’s Gini Coefficient’,* kipimo cha ugavi wa utajiri usio sawasawana umesalia kuwa 37, hali ya Uchina ni 47, na yaendelea kupanda juu – maelezo kuhusu hali hii ni kule kuendelea kupanuka na kuongeza kwa hao wenye mapato ya kati kukiwepo upungufu wa kiwango cha umasikini chini ya asili mia 14 katika mwaka wa 2007 kutoka kwa zaidi ya asili mia 75 kwenye mwaka wa 1990, mafanikio yaliyotajwa na Benki ya Dunia kuwa kampeini iliyofanikiwa sana dhidi ya umasikini. Mradi wa kitaifa wa kusambaza umeme umefikisha umeme katika asili mia 90 ya nyumba za Vietnam. Karibia watoto wote hufikia shule ya upili katika elimu yao huku theluthi mbili wakikamilisha elimu yao. Bima ya kitaifa ya wasioajiriwa yatarajiwa kuanzishwa kwenye mwaka wa 2009.

Mataifa mengine yanayoinuka kutoka kwenye migogoro na uchumi uliozorota yaweza kujifunza kutoka kwa tajriba ya Vietnam; kuzingatia kanuni sawa za kujenga uchumi zinauwezo wa kuwezesha nchi kukuza uwezo wake kiuchumi.

Jinsi imeonekana katika ujuzi wa kimataifa, ubadilishaji wa sera waweza kuboresha uwezo wa makampuni kushindana kwenye nyanja ya kimataifa. Mabadiliko katika nchi ya El Salvador yalifanyika yalijengeka kwa kukomesha vita vya wenyewe kwa wenyewe, kujiimarisha na ubinafsishaji, hata kufanya eneoI hilo kuwa la faida kwa kuekeza katika muundo msingi. Georgia na India ni mfano bora wa faida zitokonazo kwa kuondoa taratibu zisizofaa. Nayo nchi ya Vietnam yaonyesha umuhimu wa kukuza sekta ya umilikaji wa kibinafsi na kuhusika kwa raia wa nchi hiyo waliyoko ng’ambo, kama njia muhimu ya kuongezea mapato na uekezaji. Costa Rica nayo yaonyesha jinsi ya kuwa na bidhaa tofaut tofauti huku kukiwepo na sekta yenye nguvu ya bidhaa hizo. Mifano hii yote ni kielelezo cha jinsi sekta ya kibinafsi yaweza kuchochoea upungufu wa umasikini, na kwamba serikali yaweza kurahisisha mabadiliko haya.

**COSTA RICA: KUTOKA KWENYE KAHAWA HADI KWENYE ‘KOMPYUTA CHIPS’**

Uchumi wa Costa Rica umekua kwa asili mia tano kila mwaka kwa miongo mbili ilyopita, kutoka kwenye ukulima hadi kufikia teknolojia na bidhaa katika huduma; kutoka kwenye kahawa na ndizi hadi kwenye ‘*kompyuta chips’* , vifaa vya matibabu, na huduma za hali ya juu. Sasa nchi hiyo imefanyika kuwa nyumbani kwa viwanda vya hali ya juu ikujumuishwa *Intel,* inayotengeneza robo ya *kompyuta chips* zilizoko ulimwenguni. Mauzo ya nje yameinuka kufikia asili mia kumi kwa mwaka, kutoka milioni US$870 miaka 25 iliyopita hadi US$10 bilioni katika mwaka wa 2008, jambo lisilo la kawaida kwa uchumi wa watu milioni 4. Haya hayajafanyika kwa kupuuza sekta ya ukulima ambayo kwa wakati mmoja ilijumulisha theluthi mbili za mauzo ya nje. Sekta hiyo pia imefanya na kuongeza mazao yake tofautitafauti japo mauzo nje imepungua kwa asili mia 14 pekee. Costa Rica, katika ulimwengu imehifadhi sehemu yake kama ya sita katika mapato kutokana mauzo ya mazao ya kilimo nje. Somo kuu ni kwamba yote haya yamejengwa kwenye msingi wa uwazi wa biashara na mtaji, kwa kutumia akili na sera bora kama vifaa muhimu. Hakika swali la kwanza linalofaa kuulizwa kuhusu marekebisho na kukua kwa uchumi kama ilivyodhahiri katika ufanisi wa Costa Rica ni kwa nchi hizo kujiuliza: ‘Je nini tulicho bora kwacho?’

Mfululizo wa marekebisho ni tofauti tofauti kulingana na jinsi nchi imetunikiwa. Ndiposa serikali haiwezi kuwa na orodha iwezayo kutumia ili kusimamia marekebisho.

## KUPOKEA UTOFAUTISHAJI

Kuna kanuni za jumla ziwezazo kutumika kwa warekebishao, ila ni lazima ziambatane na hali maalum ya mahali pale. Baadhi ya changamoto za Afrika zi katika bara nzima: Kukuza uchumi kwa kutegemea bei ya mali ghafi, gharama ya juu kwa matumizi ya kimsingi, kutokuwepo na muundo msingi, upungufu wa watu wenye ujuzi, na kuongezeka kwa idadi ya watu.

**KUTOFAUTISHA AFRIKA**

Huenda moja wapo ya mwelekeo wa Afrika kwa zaidi ya miaka hamsini iliyopita ni uongezeko la utofauti wa maendeleo ya kiuchumi. Botswana na Mauritius zimemudu kuboresha kwa kiwango kikubwa mapato kwa kila mtu kutokana na usimamizi mzuri wa kiserikali. Nchi hizi zimeboresha maisha ya watu wake, ingawaje idadi yao ni ndogo sana na haiwezi kuwa mfano bora kwingineko.

Nchi zingine kama vile Ghana, Namibia, Msumbiji, na Afrika Kusini zimerasimisha marekebisho muhimu licha ya kutopata nyongeza katika uchumi wao. Idadi kubwa ya nchi za Afrika zimekubali kufanya marekibisho ya kiuchumi, lakini hawajarasimisha inavyohitajika ajenda za usimamizi ili kuendeleza kukuza uchumi. Uchumi wa nchi hizi zilikuwa sana hivi majuzi kutokana na mauzo ya bidhaa mbali mbali, ila sasa kutokana na kupunguka kwa bei ya mali ghafi ya kuuza nje, hali ya kiuchumi imebadilika ila si kwa kiwango kikubwa.

Kuna nchi zingine za Afrika (kama vile Demokrasia ya Kongo, Liberia, Sierra Leone, na Zimbabwe) ambazo taasisi zao za kimsingi zimeadhiriwa mno kutokana na ghasia, na usimamizi mbaya, jambo ambalo limesababisha shida miongoni mwa watu wake. Hata hivyo, kuna nchi nyingine (kama Liberia kwa mfano) zimeanza kujitoa kwenye hali kama hiyo. Mwisho ni nchi za Afrika zenye utajiri wa mafuta (kama vile Angola, Equatorial Guinea, na Nigeria) ambazo ni tofauti mno na nchi nyinginezo kwa sababu ya mauzo ya petroli inayowaletea fedha (mapato) nyingi sana hasa kwa viongozi kwa kiwango kwamba hawana motisha ya kusaidia kuwepo usimamizi bora na kuwezesha namna mbali mbali ya kutega uchumi, ingawaje mafuta hayatakuwepo kwa wingi kiasi cha kufanya nchi nzima kutajirika

Ni hali hiyo ya kuwa na namna mbali mbali ya kutega uchumi ndiyo yafaa kuiongoza Afrika katika uhusiano wake kibiashara na ulimwengu; ukosefu wa kupokea utofautishaji wa uchumi, yaonyesha jinsi hatua muhimu zilizofikiwa na serikali za Afrika huupuzwa wakati kuna maoni mengine kutoka nje ya bara hili.

Imetambulika kuwa serikali tofauti, ikijumuishwa zile zilizo na mandeleo katika kufanya marekebisho ya kiuchumi, zile ambazo ajenda zao za marekebisho hazijakamilika, na zile ziuzazo mafuta nje ya nchi zao na kupokea fedha kutokana na mauzo ya rasil mali ambatani (‘*Hydro – carbon’)* zaweza kutokubali marekebisho ya kiuchumi.

Kila moja ya serikali hizi zakumbana na changamoto tofauti katika kupunguza gharama na kuwa kakamavu. Zile ambazo tayari zimefanya marekebisho zina kazi ya kuwavutia waekezaji. Nazo nchi ambazo haizijapinga hatua kubwa ya marekebisho ni lazima kufanya bidii ya kutegemea uchumi wa kinyumbani hasa katika sekta ya rasmi. Nao wenye mafuta na rasil mali nyinginezo wafaa kuwa waangalifu sana kwamba mapato ya biashara nje haishindi uchumi na kwa kuzuia kufanyika kwa biashara kwingineko kutokana na gharama kali.

## AJENDA KUHUSU SIKU ZA USONI

### Sera Zenye Maleongo Ya Ukakamavu

Mjadala wa maendeleo hauhusu hali ya usawa kati ya serikali na soko huru, lakini habari ya kuwepo kwa soko zaidi na serikali yenye kuleta matokeo yatarajiwayo. Hili lahusu viwanda zinazomilikiwa na wenyeji au wageni, zilizoko Afrika na zashindania soko la ulimwengu.

Maendeleo yapatikanayo kwa ukakamavu yahitaji yafuatayo:

- Uchanganuzi wa gharama ya muundo wa uchumi na kujitolea kushughulikia shida zenye gharama kubwa kwanza.
- Ukakamavu wa nchi upewe nafasi ya kwanza katika mijadala yote ya kisiasa. Kukuza ukakamavu katika eneo ya nchi (Kwa mfano Afrika ya kati) na kimataifa iwe lengo kuu la kisiasa, na kutambuliwa hivyo na wapiga kura pamoja na kuwa msingi wa vyama vya kisiasa.
- Kuwepo kwa hali ya kuendelea ya kutambua sekta za uchumi ziwezazo kuwa kakamavu ikilinganishwa na hali ya uchumi wa kimataifa jinsi unavyobadilika mara kwa mara

### Yapasayo Serikali Za Afrika Kufanya

Serikali za Afrika sharti zitambue fursa za kukuza uchumi na kuhimiza mjadala wa kinyumbani kuhusu maendeleo. Ni lazima raia wa nchi kutambua kwamba wamo katika mashindano na ulimwengu wote. Hali hii yahitaji kugeuzwa kwa mawazo ya hao wanaotengeneza sera, kwa kutozingatia misaada na wafadhili, na kusisitiza biashara na uekezaji.

**ALAMA TEULE ZA UKAKAMAVU**

Kati ya mawazo yanyofaa kufikiriwa tena kuhusu maendeleo ya Afrika ni kwamba, lazima ihusishe Malengo ya Umoja wa Mataifa ya malengo ya maendeleo ya milinia (UN's Millenium Development Goals) kwa kuwepo na alama teule za ukakamavu {– mfano wa malengo ya maendeleo ya milinia (*MDGs for competitiveness)* ya ukakamavu}. Kwa kuhusisha uvumbuzi wa kiuchumi na usimamizi bora, malango kama hayo yatasaidia kuleta hali ambayo nchi zaweza kujenga na kuinua biashara na kwa kufanya hivyo, *fanya biashara wakiwa kwenye njia ya kuondoka kwenye utumwa wa umasikini.* Malengo hayo yatashughulikia ishara ambazo zingeliwazuia waekezi kufanya biashara kama vile: gharama ya mtaji, umeme, uchukuzi, mawasiliano, ushuru, wafanya kazi, na ufisadi. Itajengeka juu ya na kuunganishwa na kazi bora ya Benki ya Dunia na taasisi nyinginezo ikiwemo Jopo la Uchumi wa Ulimwengu ( World Economica Forum) katika kuorodhesha vizuizi vya kufanya biashara katika Afrika na sehemu nyinginezo za Ulimwengu.

kwa hivyo serikali za Afrika zifanye hivi:

- Waanzishe mdahalo wao wenyewe kuhusu maendeleo.
- kutoa muda zaidi kwa serikali kuhimiza uekezaji, si kujadili kuhusu jinsi ya kupokea misaada. Jenga sehemu moja itakayoshughulikia yote yanayohitajika na kurahisisha taratibu kwa ajili ya waekezaji na sio wafadhili.
- Hakikisha kwamba uchumi wote kwa jumla umejengeka kwenye kanuni na msingi dhabiti, hii yahusisha uadilifu katika hazina ya serikali, biashara na sera za kifedha
- Rahisisha kanuni za maadili mema za kufanya biashara.
- Hakikisha kwamba mabadiliko ya usimamizi na sera za ushuru zajulikana mapema.
- Ujenzi wa soko nzuri la mikopo enye uwezo wa kuwahudumia wateja wa tabaka zote, viwanda na waekezaji.
- Hakikisha kwamba kuna ukakamavu katika soko la ubadilishanaji wa fedha za kigeni

**HAKIKISHO LA SOKO KAKAMAVU YA UBADILISHANAJI WA FEDHA ZA KIGENI**

Ingawaje nchi yaweza kuwa imejimudu katika ukakamavu wa kinyumbani, bei ya bidhaa zake katika soko la kimataifa hutegemea kiwango cha ubadilishanaji wa fedha. Thamani ya fedha za kigeni ikiwa juu sana, itaondosha ukakamavu wa kinyumbani na hivyo kuzuia kuendeleza kutafuta biashara nje ya nchi. Karibia nchi zote zenye uchumi unaokuwa zilianza kufanikiwa katika uchumi wao kwa kuwa na ubadilishanaji wa fedha za kigeni ambazo thamani yake ni kakamavu na mauzo ya nje kuongezeka kwa kasi. Japani, Korea, Taiwan, Chile, Malaysia ni nchi zilizoanza kukuza uchumi wao wakati ambapo sarafu zao zilikuwa dhaifu dhidi ya fedha nyingine za kigeni. Maendeleo ya haraka ya Uchina usio wa kawaida vivyo hivyo umeungwa mkono kwa kuwepo na sarafu dhaifu hapo awali, kukua haraka katika mauzo ya nje, na kuzuia katika hali upungufu wo wote katika ukakamavu wao katika ulimwengu kutokana na sarafu yake kupata nguvu zaidi. Uchumi usioendelea wala kukua, hulaumiwa kwa kuwepo na kuongezea mno thamani ya viwango vya ubadilishanaji wa fedha katika nchi zenye bidhaa za gharama ya juu ila kwa muda tu (hiyo ndiyo "ugonjwa wa Kidachi" – tazama hapo chini), au kupokea mtaji wa muda itokanayo na riba za juu katika soko la nyumbani, au ufadhili mkuu.

Kudumisha ukakamavu katika viwango vya ubadilishanaji wa fedha yahitaji uamuzi wa kisera, kwa ufahamu kwamba jinsi mauzo ya nje ya nchi yaendelea kuongezeka ndivyo sarafu yake pia huwa na nguvu zaidi. Sera za kuzuia thamani ya sarafu isiongezeke yajumuisha Benki Kuu kununua hazina ya fedha za kigeni, kuwepo mkakati wa muda wa kushikilia mali ya kitafia nje ya nchi kwa matumizi ya baadaye, sera za kuzuia kuingizwa kwa mtaji wa muda mfupi, na kufungua soko za nyumbani ili kuhimiza uagizaji wa bidhaa kutoka nje na uekezaji nje ya nchi pia.

Zaidi, serikali za Afrika lazima kuzingatia:

- Kutambua sekta zenye faida kuu linganifu, hii ni ikiwemo utalii na huduma nyinginezo, uchimbaji wa rasil mali na manufaa yake, na kilimo.
- Kujenga muudo msingi ili kukuza uzalishaji.
- Kuondoa siasa katika sekta ya umma na kuifanya kwa wajuzi.
- Kuweka alama teule ya ukakamavu wa taifa – dhidi ya ulimwengu
- Kuondosha ukiritimba – hasa makampuni yaendeshwayo kwa ushawishi wa kisiasa – na kutanguliza mahitaji ya watumizi mbele ya manufaa ya mzalishaji; hili hufanya wazalishaji wa bidhaa kuwa wakakamavu.
- Kupunguza gharama ya kurasimisha na gharama ya kufanya biashara kwenye sekta ya kibinafsi, huku gharama ya sekta isiyo ya kawaida ikipanda katika utekelezaji wa biashara.
- Kuunda daraja kati ya Waafrika walioko ng'ambo badala ya kuomboleza kuhusu uhuamiaji wa wataalamu. Wataalamu hao wahitaji kushirikishwa katika kuboresha ukakamavu wa nchi za Afrika kwa teknolojia, , usimamizi wa fedha, ujuzi, na pia kuwa waakilishi/mawakili wa Afrika huko waliko hamia. Katika Amerika Kaskazini pekee, kwa mfano, kuna karibia wahamiaji kutoka Afrika milioni 1.3. Wao waakilisha asili mia 3.6 ya wakaazi wa Marekani waliozaliwa nje ya nchi hiyo, huku idadi yao ikiwa asili mia 17.7 ya wahamiaji halali tangu mwaka wa 2000.
- Kubuni 'Kilimo kipya', ila kuwa wazi kabisa ni muhimu kujua ni jinsi gani litaungwa mkono na uekezaji utakuwaje ili ufanisi uwepo.

**MTAZAMO WA AFRIKA KWA 'KILIMO KIPYA'**

Licha ya kutunikiwa kwa rasil mali, nchi za Afrika kama tamaduni, sekta yake ya kilimo katika ulimwengu wote ndiyo huwa mbovu bila ya mazao kama itarajiwavyo. Kwa sababu hiyo, kati ya nchi 48 zilizoko kusini mwa Sahara, 35 kati yazo huagiza chakula kutoka nje. Kwa mfano, nchi za Afrika Mashariki zimeongeza mara tatu mazao ya kilimo katika miongo nne iliyopita, Afrika imesalia nyuma, mazao yakiwa zaidi au bila nyongeza.

Uzalishaji wa chini wa mazao pamoja na muundo msingi mbaya na soko dhaifu la nyumbani ni tisho kubwa kwa maendeleo ya Afrika katika kuuza mazao katika miji. Gharama ya juu ya chakula imekuwa yenye madhara makubwa na kichocheo cha hali ya wasi wasi ya kisiasa, hasa katika miji. Hata hivyo, mengi yamejulikana ya jinsi ya kutengeneza hali nzuri ya 'mageuzi ya kijani kibichi' (Green Revolution). Wadhfa wa Rockefeller ulifanya mhutasari kwa yanayohitajika. Nao ni kama ifuatavyo:

- Kuza mimea yenye mazao ya juu, na kutengeneza mbolea kwa kutumia utafiti;
- Utumizi wa talanta za wenyeji katika sayansi ya kupanda, sera za kilimo, na biashara;
- Kujitolea kwa serikali ya kitaifa.
- Ushirikiano wa sekta ya umma na ya kibinafsi kuhusu muundo msingi, maji, unyunywizaji wa maji, na mazingira, na
- Kujenga masoko

Uhusiano wa moja kwa moja kati ya kilimo na biashara ni lazima kusisitizwa. Karibia nusu ya nchi zilizoko kusini mwa Sahara, malipo ya uchukuzi huchukua asili mia 20 ya mapato yote ya kigeni kutoka kwa mauzo ya nje. Kwa nchi zisizo kwenye ufuo wa bahari, gharama hii hufikia asili mia 50. Hasa kuu katika yasababishayo gharaham hizi kuwa za juu ni miuundo msingi mbaya wa uchukuzi mashambani, jambo linalofanya wakulima wa Kiafrika kukuza mimea yenye bei ya juu kwa ajili ya soko la kimataifa. Hili halihusishi tu malipo kwa matumizi ya uchukuzi, kwa sababu ya miuundo msingi mbaya bali gharama ya kufanya biashara pia inayosababishwa na idara za forodha na utaratibu wa kuondosha mizigo zisizofanya kazi vyema, zenyewe zikiwa sehemu na matokeo ya kulazimishwa na urasimu usiofanya kazi vyema, mawazo yasikokuwa na ukakamavu, na sera za mazingira.

Nyongeza ya bei ya vyakula, hali ambayo uwekano wa kurekebishwa haupo, yaifanya Afrika kukabili kweli kinza ikiunganishwa na wasi wasi wa kisiasa, na, iwapo kilimo kitafufuliwa, basi nafasi za kukuza uchumi zitakuwepo kwa wakulima wadogo wadogo wapatao 180 milioni. Itakuwa janga kuu sana iwapo hali ya wasi wasi itashughulikiwa kisha fursa ya kuinua uchumi ipitwe bila kuonwa.

## Wajibu Wa Sekta Ya Kibinafsi Na Watendaji Wasio Wa Kiserikali

Ukakamavu wa taifa hutegemea sera za serikali na utekelezaji wazo. Lakini mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), taasisi na wafadhili waweza kusaidia.

Umma waweza kuchochea mabadiliko na kufanya kazi ya angalia kwa umaakini matumizi ya mamlaka lakini pia kuna hitaji la mashirika ya umma kufanya yafuatayo:

- Nyosha na kukubali kanuni ya maadili mema ya kufanya biasha, na kwa mashirika mengine kama hayo yasiyokuwa ya kiserikali (NGO), yakiangalia hitaji la kitaifa la ukakamavu mkuu kwa kupunguza gharama ya kufanya biashara.
- Kuhusika zaidi katika elimu ya uchumi, na kuunga mkono waekezaji wa kibinafsi kukuza mipango ya biashara zao.
- Elimisha watunga sheria na wafanya kazi wa bunge kuhusu usimamizi halali wa mazingira yaruhusuyo ukakamavu wa biashara
- Kuonyesha jinsi watumizi, wafanya kazi, na mazingira waweza kulindwa bila ya kufanya gharama ya kufanya biashara kuwa zuilifu
- Zingatia sera zihusuzo pengo liliko kati ya mijini na mashambani.

## Jinsi Misaada Zaweza Kusimamiwa Vyema.

Kwa kuwa maendeleo ni hatua za kisiasa, ufanisi wake wategemea umiliki wa kinyumbani; yabidi watengenezaji sera wa Afrika kutunga aula za kwanza, na si wafadhili. Aula za kwanza ni lazima kutambuliwa kulingana na hali ya kipekee ya kila nchi. Ilikuwepo na usawa kati ya hitaji la serikali na kile wafadhili wataka kutoa, ni lazima wafadhili:

- Kuunga mkono kukuzwa kwa uchumi wa kitaifa na ajenda za kupunguza gharama, huku wakiepuka hali ya kuzitenezea nje au kutafuta sera ‘kamilifu’.
- Pamoja na taasisi za usimamizi wa fedha za kimataifa, ni vyema kuwa waangalifu wasizuie serikali kutumia fedha kwa hayo ya kimsingi katika yaendelezayo uchumi.
- Shirikiana na seka ya kibinafsi katika kuunda muundo msingi

Tambua na kusitisha misaada nyingine iwezayo kuingizwa katika nchi yenye madhara kwa maendeleo yaliyopo, ikiwemo ule ‘Ugonjwa wa Kiholanzi’ (Dutch Disease) na kupanda kwa thamani katika viwango vya kubadilisha fedha zielekeazo kwa rasil mali za mfadhili badala ya mahitaji na matarajio ya biashara.

**KUEPUKA ‘UGONJWA KIHOLANZI’ (DUTCH DISEASE)**

Jina hilo ‘ugonjwa wa Kiholanzi’ ulitokana na hali iliyokuwako katika nchi hiyo kwenye miaka ya 1960 kutokana na uvumbuzi wa kuwepo kwa mafuta katika Bahari ya Kaskazini, iliyofanya sarafu ya Kiholanzi kupanda jambo lililofanya bidhaa zisizo za mafuta kutokuwa na ukakamavu katika soko la ulimwengu. Hali hii ilitukia Uingereza pia katika miaka ya 1970 kwa msingi uo huo. Hali ugonjwa huo wa Kiholanzi ulishirikisha matokeo ya rasil mali, na ni ya kufikiriwa sana hasa kuhusu nchi za Afrika zenye utajiri mkubwa, maana zaweza kuleta mapato mengi ya pesa za kigeni, ikiwemo uekezaji wa moja kwa moja na misaada ya wafadhili.Matokeo ya ongezeko la uagizaji wa bidhaa na kupungua kwa mauzo nje, kutokana na nyongeza katika uhalisi wa ubadilishanaji wa fedha za kigeni yaweza kusababisha kazi za kutengeneza bidhaa kuhamishwa hadi nchi zenye gharama ya chini ya kibiashara

Kuna njia tatu mwafaka za kuzuia ugonjwa kiholanzi:

Kwanza, ni kwa kusitiza hali halisi ya kiwango cha ubadilishanaji wa fedha za kigeni kwa kutoingiza mapato yote mara moja katika nchi, hivyo kuziweka kama hazina au kuzitumia kwa njia ambayo itahakikisha udhabiti wa kuingiza mapato. Mkakati wa pili ni kuzuia uhalisi wa ongezeko la kiwango cha ubadilishanaji wa fedha za kigeni ni kuongezea katika hazina ya kinyumbani katika uchumu kusudi ipunguze kiwango kikubwa cha kuingizwa kwa mtaji. Hili laweza kufanyika katika nchi yenye masalio ya bajeti. Nchi yaweza kuhimiza watu binafsi na viwanda kuweka hazina kwa kupunguza mapato na ushuru na faida. Kuweka hazina kutapunguza pakubwa hitaji la mikopo kwa serikali ili kuongezea katika upungufu ulioko na uekezaji wa kigeni. Njia ya tatu ni kuinua hali ya ukakamavu katika sekta ya kuunda bidhaa, kwa kuongeza uekezaji katika elimu na muundo msingi.
Kwa jumla, usimamizi bora ndio suluhu ya ugonjwa wa kiholanzi. Kwa kuhakikisha kuwa kuna kanuni bora za kiuchumi, basi sarafu haiwezi kuwa na thamani ya juu au kutafuta kodi: Sera bora za usimamizi wa fedha, uwazi katika kufanya biashara na utawala wa uekezaji, sheria za uwazi katika utendaji kazi kupitishwa, sheria dhidi ya ufisadi, utawala wa sheria, na uekezaji wa muda mrefu miongoni mwa watu, afya na muundo msingi.

## KUELEKEA AFRIKA KAKAMAVU

Afrika yaweza kujifanyizia njia ya ufanisi wa kiuchumi kwa kuunda ‘muungano wa kukuza uchumi’ barani. Hii ni changamoto ya kipekee: Afrika ni lazima ikamilishe viunzi vya marekebisho na uekezaji wa umma kwa muda mfupi sana, ikilinganishwa na historia ya jinsi uchumi wa Ulaya ulivyokua au ule wa Asia. Zaidi ni kwamba, Afrika lazima ifanye hivyo wakati ambapo kuna msukosuko katika uchumi wa ulimwengu.

### KUUNDA MIUUNGANO YA KUKUZA UCHUMI AFRIKA

Uchumi wa Afrika kwa kiwango kikubwa umetegema bei ya bidhaa katika soko la kimataifa. Hivyo ina safari ndefu sana ya kuwa msukumo ikizingatiwa hali yake ya kimaendeleo na utumizi wa mtaji wa kibinadamu kwa mazao yahitajikayo katika soko la ulimwengu – dereva wa muda mrefu wa kukuza uchumi uliodhibitika kwingineko

Kuna hitaji la mabadiliko, japo kila nchi imejawa mashirika mbali mbali akilishi, hayo yasiyo ya kiserikali (NGOs) taasisi za maendeleo, Waelekezi na serikali za kigeni. Kelele hizo nyingi zaweza kuchanganya na kuelekeza vibaya na mara nyingi hufanyika kuwa udhalilishaji wa kisiasa badala kuwa kama ilivyotarajiwa chimbuko la mapato ya kufanya maendeleo na ushauri. Badala ya kuzingatia ukuzaji wa uchumi, taasisi hizi hupofusha viongozi wa kisiasa wasione shida kama zilivyo.

Ulimwengu sasa u katika muongo wa tano katika mstari wa mbele wa kimataifa katika kuisaidia Afrika kimaendeleo huku mifano ikifuatwa. Mifano hii yatokana na hali moja ya fikra na utendaji wa mashirika makuu ya kimataifa ya kutoa misaada. Kwa jumla, twaweza kusema kuwa historia ya usaidizi wa maendeleo kwa muhtasari ni ufanisi unaoendelea wa kutoa rasil mali (Miaka ya sitini hadi katikati mwa miaka ya themanini), kubuni sera (Miaka ya katikati ya themanini hadi mwaka wa elfu mbili) na kwa kuinua uwezo wa kutekeleza sera hizo (Kutoka kwenye mwaka wa 1995 – 2005). Katika miaka michache ya nyuma, mtazamo umerudia habari ya rasil mali kwa mtindo wa kubainisha malengo kama ilivyo afikiwa katika jopo za kimataifa, kuelekea bajeti kubwa ihusishayo eneo lote

Kuna kila uwezekano wa hali hii kuendelea, huku matokeo yakitabiriwa kwamba yatakuwa ya kuvunja moyo. Sababisho haitatokana na mawazo pungufu au kasoro ya kiuchumi kwa upande wa wafadhili wakuu: rasil mali, sera, na uwezo wa utekelezaji wahitajika maana ndio vifaa ambavyo kwavyo uchumi wakuzwa na kufaulu. Lakini iwapo viongozi wa nchi watakuwa na aula za kwanza nyingine, yote haya hayatazalisha cho chote.

Hiyo ndiyo kiuungo kisichokuwepo: Aula za kwanza miongoni mwa vikundi vya viongozi. Ukuzaji wa uchumi ukiwa ndiyo aula ya kwanza, rasil mali yaweza kukusanywa, sera kuandikwa, na suluhu mpya kuwasilishwa itakayowesha utekelezaji. Iwapo aula nyinginezo ndizo zitapewa kipaumbele, basi ukuzaji wa uchumi hupata pingamizi kwa kiwango kwamba hakuna atokaye nje aweza kuelewa. Yote haya yaonyesha shida ya aula ya kwanza iliyopewa ukuzaji wa uchumi, ambayo huonyesha kwamba muungano uliopo unaotawala aual zao za kwanza zimepewa vitu vingine na si ajenda yu kukuza uchumi. Nia ya kisiasa daima huwa imechanganya mambo, ila ni katika nchi ambayo kuna muungano wenye nguvu kwa ajili ya kukuza uchumi, ndipo sera ya umma ya kukuza uchumi hufuatiliwa kwa ujasiri na uhodari ili kutekelezwa.

Kwa hivyo si jambo la kushangaza kwamba mashirika ya kigeni hushindwa kutengeneza muungano wa kukusan uchumi. Kimsingi mashirika kama yale huwa ya kutoka kwenye serikali bingwa na miiko ya uenzi, huku ujenzi wa muungano ni zoezi la kisiasi katika mashina yake

Ufanisi na udhabiti wa Afrika utapatikana kwa njia hii ya kipekee, hapo serikali itakapoachilia huru waekezaji na kuanza kuelewa ni nini hicho walicho nacho cha kuuzia ulimwengu kuliko vile mataifa mengine yaweza kuuza. Ufanisi utahitaji utekelezi wa serikali: Uekezaji mkubwa katika watu na mtaji wa miuundo msingi, pamoja na sera zinazozingatia kupunguza gharama na vizuizi vya kufanya biashara

Ni lazima wafadhili kujizuia hali ya kujibu maswali muhimu kwa niaba ya Afrika. Cha muhimu ni kile Afrika yaweza kujifanyia, hata kama itaonekana kuwa ni chini ya kile inachoweza kufanyiwa. Ni serikali tu za Afrika zikifanya kazi na wafanya biashara, watunga sheria, na umma, ndipo muungano wa kisiasa utajengeka nao ndio utahitajika katika barabara hii ngumu na ndefu ya maendeleo.

Katika nchi nyingi za Afrika, mjadala kuhusu marekebisho na ufanisi hayajaanza bado. Maufaka wa Ziwa Kivu ni hatua katika ngazi hiyo.

* * *

## Appendix: Participants*

| | |
|---|---|
| Alan Gelb | World Bank: Washington DC, South Africa |
| Alberto Trejos | INCAE, Costa Rica |
| Alex Sokoloff | US Embassy: Rwanda, United States |
| Andres Rozental | Council on Foreign Relations, Mexico |
| Andrew Rugasira | Good African Coffee, Uganda |
| Ann Bernstein | Centre for Development Enterprise, South Africa |
| Annette Schwarzbauer | Konrad Adenauer Stiftung, Germany |
| Antoinette Mokgohloa | Pamuzinda Productions, South Africa |
| Anton Bosl | Konrad Adenauer Stiftung: Namibia, Germany |
| Betty Maina | Association of Manufacturers, Kenya |
| Casper Klynge | Africa Commission, Denmark |
| Dan Makokera* | Pamuzinda Productions, Zimbabwe |
| Dianna Games | Africa@Work: South Africa, Zimbabwe |
| Erastus Mwencha | Commission of the African Union: Ethiopia, Tanzania |
| Fatima Harrak | Institute of African Studies, University of Mohammed V, Morocco |
| Frank Spengler | Konrad Adenauer Stiftung, Germany |
| Greg Mills* | The Brenthurst Foundation, South Africa |
| Holger Hansen* | Centre of African Studies, University of Copenhagen, Denmark |
| Hyuha Mukwanason | African Economic Research Consortium: Kenya, Uganda |
| James Kibera* | Mzima Ltd, Kenya |
| Jeffrey Herbst* | Miami University, United States |
| Jennifer Oppenheimer | The Brenthurst Foundation: South Africa, United States |
| John Williamson | Peterson Institute for International Economics, United Kingdom |
| Jonathan Oppenheimer | DB Investments, South Africa |
| Kipyego Cheluget | Foreign Service Training Institute, Kenya |
| Klaus Rudischhauser | European Commission: Brussels, Germany |
| Mark Bellamy | African Center for Strategic Studies, United States |
| Markus Lackamp | Political Programmes and Analyses: Christian Democratic Union, Germany |
| Martin Kimani* | *The East African*, Kenya |
| Mauro De Lorenzo* | American Enterprise Institute, United States |
| Michael Spicer* | Business Leadership SA, South Africa |
| Mohammed Dahbi | Al Akhawayn University, Morocco |
| Morten Elkjaer | Africa Commission, Denmark |
| Mundia Kabinga | University of the Copperbelt, Zambia |
| Natty B Davis | Presidential Adviser and Minister, Liberia |
| Patrick Mazimhaka* | The Brenthurst Foundation, Rwanda |
| Paul Kagame | President, Rwanda |
| J Peter Pham* | James Madison University, United States |
| Peter Zeng | Chinese Institute for Contemporary International Relations, China |
| Robert Sithebe* | KPMG, Swaziland |
| Sheila Khama | De Beers, Botswana |
| Simon Rutega | Uganda Securities Exchange, Uganda |
| Stefan Mair | Stiftung Wissenschaft und Politik, Germany |
| Stephan Malherbe* | Genesis Analytics, South Africa |
| Stephen Karingi | UN Economic Commission for Africa: Ethiopia, Kenya |
| Steve Caley | Fina Bank: Rwanda, United Kingdom |
| Stuart Symington | Ambassador to Rwanda, United States |
| Tan Khee Giap | S Rajaratnam School of International Studies, Singapore |
| Terence McNamee* | Royal United Services Institute: United Kingdom, Canada |
| Thomas Claiborne | E Oppenheimer & Son: South Africa, United States |
| Thomas Nzaritimana* | TransAfrika Resources: South Africa, Democratic Republic of Congo |
| Thomas Vester Nielsen | BankInvest, Denmark |
| TN Ninan | *Business Standard*, India |
| Tumenta Kennedy | Wittenberg Center for Global Ethics: Germany, Cameroon |
| Victor Ngezayo | Group Ngezayo, Democratic Republic of Congo |
| Witney Schneidman | Schneidman and Associates, United States |

* Denotes attendance at both meetings in Como and Kivu in May and December 2008 respectively; no asterisk denotes participation at one meeting only. The last-named country refers to the participant's national origin.